

## Msaada wa kodi ya COVID-19 unapatikana

Ikiwa umechelewa kulipa kodi yako au uko katika hatari ya kufukuzwa, unaweza kuomba msaada wa kodi ya kufukuzwa au kutafuta msaada kutoka kwa mpango wa utatuzi wa kufukuzwa.

Wamiliki wa nyumba hawawezi kutoa ilani za kufukuzwa kwa sababu ya kuchelewa kulipa kodi kutokana na janga la COVID-19 isipokuwa iwango vitu hivi vitatu ni kweli:

- Kuna mpango wa uendeshaji wa usaidizi wa kodi katika kaunti unamoishi. Wasiliana na mtoa huduma katika kaunti yako kwa taarifa kuhusu jinsi ya kuomba. Orodha: <https://www.commerce.wa.gov/serving-communities/homelessness/eviction-rent-assistance-program/>
- Kuna mpango wa uendeshaji wa utatuzi wa kufukuzwa katika kaunti unamoishi. Orodha: <https://www.resolutionwa.org/locations>
- Mmiliki wa nyumba yako amejaribu kushirikiana nawe kuomba usaidizi kupitia mojawapo ya mipango hii.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu (Office of the Attorney General) inaweza kusaidia na malalamiko yanayohusiana na kufukuzwa kutoka kwa wapangaji na wamiliki wa nyumba. <https://fortress.wa.gov/atg/formhandler/ago/COVID19EvictionComplaintForm.aspx>

## Nyenzo zinapatikana ili kusaidia matumizi mengine—Piga simu 2-1-1 kwa ajili ya taarifa

Tembelea [wa211.org](http://wa211.org) au piga simu 2-1-1 ili kuongea na mtu ambaye anaweza kutoa taarifa ya kusaidia watu kulipia vitu kama bili za nishati, chakula, muunganisho kasi wa tovuti na kadhalika.